

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA HAMSINI NA TANO

27 JUNI, 2024



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

### MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA HAMSINI NA TANO – TAREHE 27 JUNI, 2024

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):**

Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Tume ya Utumishi wa Umma kwa kipindi cha Julai, 2022 hadi Juni, 2023.

**WAZIRI WA FEDHA:**

Maelezo ya Waziri wa Fedha kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2024 (*The Finance Bill, 2024*).

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2024 (*The Finance Bill, 2024*).

### **III. MASWALI:**

#### **OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

##### **706. MHESHIMIWA DEODATUS PHILIP MWANYIKA (NJOMBE MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itapeleka Vifaa Tiba katika Vituo vya Afya vya Kifanya na Makowo vilivyojengwa kwa nguvu za Wananchi.

#### **OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

##### **707. MHESHIMIWA ASHA ABDULLAH JUMA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kudhibiti matumizi ya vifuko vya plastiki.

#### **WIZARA YA NISHATI:**

##### **708. MHESHIMIWA MUHARAMI SHABANI MKENGE (BAGAMOYO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, lini Mradi wa Umeme katika eneo la Kitume Kata ya Makurunge - Bagamoyo utaanza kujengwa.

## **WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:**

### **709. MHESHIMIWA OMAR ISSA KOMBO (WINGWI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum:-

Je, Serikali ina mikakati gani ya kukabiliana na vitendo vya ukatili ikiwemo mauaji yanayotokea kwenye jamii kwa sababu za wivu wa kimapenzi.

## **WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

### **710. MHESHIMIWA NORA WAZIRI MZERU (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia Wasichana wanaokatisha Masomo kwa sababu ya kupata ujauzito.

## **WIZARA YA FEDHA:**

### **711. MHESHIMIWA DKT. FAUSTINE ENGELBERT NDUGULILE (KIGAMBONI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanza kwa matumizi ya Sarafu za Kidijitali (*Central Bank Digital Currency*) hapa nchini.

## **WIZARA YA KILIMO:**

### **712. MHESHIMIWA EMMANUEL PETER CHEREHANI (USHETU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Maghala ya kuhifadhi Mazao katika Halmashauri ya Ushetu.

## **WIZARA YA UJENZI:**

### **713. MHESHIMIWA IDDI KASSIM IDDI (MSALALA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara ya Chela - Busengi hadi Kahama kwa kiwango cha lami.

**714. MHESHIMIWA SAMWELI XADAY HHAYUMA (HANANG'):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, Serikali imefikia hatua gani ya ujenzi wa Barabara ya Haydom hadi Mogitu kwa kiwango cha lami.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**715. MHESHIMIWA MWATUM DAU HAJI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, kuna mpango gani wa kuongeza kasi ya ujenzi wa Vituo vya Polisi nchini.

**IV. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:**

*(Kusomwa Mara ya Pili, Kamati ya Bunge Zima na Kusomwa Mara ya Tatu)*

Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2024 (*The Finance Bill, 2024*).

**DODOMA  
27 JUNI, 2024**

**N.J. MWIHAMBI, ndc  
KATIBU WA BUNGE**